# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO MHESHIMIWA FREDERICK T. SUMAYE (MB.), WAKATI AKIWASILISHA MAKADIRIO YA WIZARA MWAKA 1995/96

I. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya matumizi, ili liweze kujadili na hatimaye kuidhinisha makadirio ya Wizara ya kilimo kwa mwaka 1995/96.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Cleopa David Msuya (Mb.) kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais. Aidha nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jackson M. Makwetta (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini na kumshukuru kwa kazi nzuri aliyoifanya wakati akiwa Waziri wa Kilimo. Mimi na wenzangu katika Wizara tumefaidika sana kutokana na misingi aliyoweka. Vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Njelu M. Kasaka (Mb.) aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo. Ninamkaribisha kwa moyo mkunjufu Wizarani. Pia napenda kumpongeza Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais na Mawaziri wenzagu walionitangulia kusoma hotuba zao ambazo zimefafanua masuala mengi yanayohusu kilimo. Michango ya Wabunge nayo imesaidia sana kuonyesha maeneo yanayohitaji msisitizo katika Wizara yangu.

3. Mheshimiwa Spika, taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) ya mwezi Februari mwaka 1995 inaonyesha kuwa ili kukidhi mahitaji ya chakula duniani kwa mwaka 1995/96, uzalishaji wa nafaka utatakiwa uongezeke kwa asilimia 4. Hata hivyo lengo hilo litakuwa vigumu kufikiwa kwa sababu ya mabadiliko ya sera, hasa yanayohusu kupunguzwa kwa ruzuku kwa wazalishaji na wauzaji nje katika nchi mbalimbali. Katika hali hii ni dhahiri kuwa waagizaji wa nafaka kutoka nje, itabidi walipie gharama kubwa zaidi hasa kwa zao la ngano.

4. Bara la Afrika, hasa katika nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara (Sub-Saharan Africa) zitakabiliwa na tatizo la uhaba wa chakula. Upungufu huu unasababishwa na ukame ambao umekuwepo kwa misimu minne

mfululizo katika baadhi ya nchi, magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea na mazao, bei kubwa za pembejeo, teknolojia duni na milipuko ya vita vya wenyewe kwa wenyewe.

5. Baadhi ya nchi za SADC kama Botswana, Lesotho, Malawi, Mozambique, Nambia, Swaziland, Zambia na Zimbabwe zimeathiriwa na ukame uliotokana na mvua kidogo ambayo pia ilichelewa kunyesha na kukatika mapema. Katika nchi hizi uzalishaji wa mahindi unakisiwa kuwa umeshuka hadi tani 11.87 milioni kwa mwaka 1994/95 ikiwa ni upungufu wa asilimia 41 ikilinganishwa na mavuno ya msimu wa mwaka 1993/94. Kwa upande wa Tanzania uzalishaji wa mazao makuu ya chakula kwa mwaka 1994/95 unaonyesha ongezeko la asilimia 8.7 ikilinganishwa na msimu uliopita (Jedwali Na.1).

6. Mheshimiwa Spika, upatikanaji na uzalishaji wa mazao mengi ya biashara duniani umepungua kutokana na sababu mbalimbali zifuatazo:-

- Uzalishaji wa zao la kahawa ulipungua kutokana na hali mbaya ya hewa (baridi kali na ukame) huko Brazil.
- Uzalishaji wa pamba umepungua kufuatia kusambaratika kwa Jamhuri ya Urusi na vile vile China kuzuia mauzo ya pamba nje.
- Uzalishaji wa korosho umepungua huko India hali ambayo imesababisha nchi hiyo kushindwa kukidhi mahitaji yake.
- Zao la chai limeshuka kutokana na ukame uliotokea India, Kenya, Malawi na vita vya wenyewe kwa wenyewe Sri Lanka, na
- Zao la Tumbaku limeshuka uzalishaji kutokana na ukame huko Zimbabwe na Malawi.

Hali hii ya kupungua uzalishaji imefanya bei za mazao ya kahawa, pamba, korosho, chai kuanza kuonyesha dalili za kuongezeka.

## II. MAPITIO YA MWAKA 1994/95

7. Mheshimiwa Spika, hali ya chakula katika msimu 1994/95 hapa nchini haikuwa nzuri. Sababu kubwa ya upungufu huu ni kushuka kwa uzalishaji

katika msimu uliopita uliotokana na ukame. Aidha wakimbizi kutoka nchi jirani za Rwanda na Burundi waliongeza hali mbaya ya chakula hasa katika mikoa ya Kagera na Kigoma.

8. Uhaba huo wa chakula ulidhibitiwa kwa serikali kutangaza hali ya njaa na kuwaomba wafadhili na wafanyabiashara kutoa mchango wao kwa kuleta chakula kutoka nje. Jumla ya tani 74,000 za chakula zikiwemo tani 64,500 za mahindi na tani 9,500 za mchele zilitolewa na wahisani na wafanyabiashara binafsi waliagiza jumla ya tani 104,300 za chakula zikiwemo tani 200 za mahindi, tani 38,600 za mchele na tani 65,500 za ngano. Wakati huo huo serikali ilitumia tani 95,000 za mahindi kutoka kwenye akiba yake ya tahadhari (SGR).

9. Mheshimiwa Spika, ningependa kutumia nafasi hii kuzishukuru nchi zilizotusaidia chakula zikiwemo Japan, Uingereza, Marekani, Canada, Ubelgiji, Ufaransa, Sweden, China na Mashirika mbalimbali hasa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Jumuia ya nchi za Ulaya (EU) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO). Aidha kwa niaba ya serikali napenda kuyashukuru mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) kwa mchango wao mkubwa wa kuhakikisha upatikanaji wa chakula kwa walengwa. Napenda pia kuwashukuru wakulima na wafanyabiashara waliothubutu kuingia katika eneo hili la biashara.

10. Kama nilivyodokeza awali, uzalishaji wa chakula kwa mwaka 1994/95 utaongezeka ikilinganishwa na msimu uliopita. Hali nzuri ya uzalishaji imetokana na kunyesha mvua za kutosha na kwa wakati unaostahili, pamoja na kupatikana kwa mbolea ya kutosha kwa wakati unaofaa, na ongezeko katika maeneo yaliyolimwa.

11. Mheshimiwa Spika, Makisio ya awali yanaonyesha kwamba uzalishaji wa mazao aina ya nafaka utaongezeka kwa asilimia 14.4 na yale yasiyo nafaka yataongezeka kwa asilimia 0.3. Zao la mahindi linatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 21.6, mtama na uwele kwa asilimia 23.1, ngano kwa asilimia 41.7, na zao la mpunga linakisiwa kuongezeka ukilinganisha na msimu uliopita. Uzalishaji wa sukari umepungua kwa asilimia 12.3 kutokana na:

- Uchakavu na uharibifu wa mitambo.
- Kushuka kwa uzalishaji wa miwa kulikosababishwa na wadudu waharibifu.

12. Mahitaji yetu ya chakula kwa mwaka 1995/96 yanakisiwa kuwa tani 4.113 milioni za nafaka na tani 2.539 za mazao mengine. Hii ni jumla ya tani 6.652 milioni za chakula, na zinakidhi tu mahitaji yetu ya chakula.

13. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazao ya biashara, kulikuwa na ongezeko katika uzalishaji wa korosho kwa asilimia 29, tumbaku kwa asilimia 33 na mkonge kwa zaidi ya asilimia 3. Ongezeko la korosho limetokana na ongezeko la matumizi ya "sulphur" katika kuzuia ugonjwa wa ukungu, utunzaji bora wa mikorosho, upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima na bei nzuri anayolipwa mkulima. Kwa upande wa tumbaku uzalishaji umeongezeka kwa sababu ya bei ya kuridhisha aliyopata mkulima katika msimu uliopita na kupatikana kwa pembejeo kwa wakati zilipohitajika. Uzalishaji wa zao la chai umeongezeka kutokana na kunyesha mvua za kutosha katika maeneo mengi yanayolimwa chai, pamoja na matumizi mazuri ya mbolea. Aidha bei nzuri ya zao la chai imesaidia kuhamasisha wakulima kuimarisha kilimo cha zao hilo.

14. Uzalishaji wa pamba, kahawa, na pareto ulishuka kwa asilimia 19 kwa zao la pamba, asilimia 13 kwa zao la kahawa, na asilimia 32 kwa zao la pareto. Uzalishaji pamba na kahawa ulipungua kutokana na hali mbaya ya hewa (ukame), kuchelewa kupatikana kwa pembejeo, pamoja na bei ndogo walizolipwa katika misimu ya nyuma. Kushuka kwa zao la pareto kunatokana na kukosekana kwa soko la uhakika kwa zao hili jambo ambalo lilisababisha wakulima kutolipwa kwa wakati (Jedwali Na. 2).

15. Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo kwa kipindi cha 1994/95 inatarajiwa kuwa nzuri hasa kutokana na maeneo mengi kupata mvua za kutosha. Hali hii itaifanya mifugo kuwa na afya ya kuridhisha kutokana na kupatikana kwa malisho na maji. Ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa wafugaji wadogo wadogo uliendelea vizuri. Miradi ya ng'ombe wa maziwa katika mikoa ya Iringa, Kagera, Mbeya na Tanga ilitekelezwa, na kufanya idadi ya wafugaji waliojiunga na miradi hiyo kuongezeka kutoka wafugaji 4,898 mwaka jana hadi kufikia wafugaji

5,968 mwaka 1994/95 katika mikoa hiyo.

16. Katika msimu huu jumla ya tani 219,000 za nyama na lita milioni 590 za maziwa zilizalishwa ikilinganishwa na tani 227,000 za nyama na lita milioni 555 za maziwa kwa msimu uliyopita (Jedwali Na. 3).

Aidha ukusanyaji wa ngozi ulikuwa mzuri kuliko ule wa mwaka 1993/94 na jumla ya ngozi milioni 3.861 zilikusanywa ikilinganishwa na ngozi milioni 2.85 zilizokusanywa msimu uliopita.
Kati ya hizo ngozi za ng'ombe zilikuwa milioni 1.5, za mbuzi milioni 1.8 na za kondoo milioni 0.561, na jumla ya ngozi milioni 3.596 ziliuzwa nchi za nje na kulipatia taifa shilingi bilioni 7.5.

17. Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji kuku nchini imekuwa ikiendelea vizuri licha ya kushuka kwa uzalishaji kwenye mashirika ya umma hususan Kampuni ya Kuku ya Taifa (NAPOCO). Sekta binafsi imetoa mchango mkubwa kuziba pengo hili. Uzalishaji wa vifaranga umeongezeka kutoka milioni 5 hadi milioni 7.4, na uingizaji vifaranga toka nje umepungua toka vifaranga milioni 2.4 hadi milioni 1.3.

18. Tatizo lililojitokeza katika msimu huu ni milipuko ya magonjwa, hasa ugonjwa wa homa ya mapafu ambao umejitokeza kwenye mikoa ya Morogoro, Mara, Rukwa, Kigoma, Tabora, Kagera na Arusha. Hadi mwezi Aprili, 1995 zaidi ya ng'ombe 14,000 wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 800 walikwisha kufa kwa ugonjwa huu. Hali hii inakadiriwa kusababisha upungufu mkubwa wa idadi ya ng'ombe na hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo. Wizara yangu imekwisha chukua hatua kadhaa ili kupambana na ugonjwa huu wa hatari, kama ifuatavyo:-

- kuelimisha wananchi juu ya dalili na athari za ugonjwa huu.

- kuweka karantini na kutoa chanjo katika maeneo yaliyoathiriwa na yale yanayopakana nayo.

- kutaarifu nchi jirani na mashirika ya kimataifa yanayohusika kwa ajili ya tahadhari.

19. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa msimu wa 1994/95 umekuwa wa kuridhisha isipokuwa usambazaji kwa wakulima haukuwa mzuri. Hadi mwishoni mwa mwezi Aprili 1995 jumla ya tani 209024 za aina mbalimbali za mbolea zilikuwa tayari zimekwishapatikana kwa ajili ya msimu, ambazo ni sawa na asilimia 80 ya makisio ya mahitaji. Aidha hadi kufikia mwishoni mwa Aprili 1995 jumla ya tani 115,000 zilikwisha sambazwa kwa wakulima ambazo ni asilimia 55 ya mbolea iliyopatikana.

20. Kiasi kilichosambazwa ni kidogo ikilinganishwa na miaka ya nyuma kwa sababu matumizi ya mbolea sasa yamepungua kutokana na sababu zifuatazo:

- Bei kubwa ya mbolea baada ya kufutwa ruzuku.
- Bei za mavuno kutoongezeka sambamba na kuongezeka kwa bei ya mbolea.
- Hali mbaya ya hewa hasa ukame kwenye baadhi ya maeneo.
- Kukosekana kwa mikopo ya pembejeo kwa wakulima wadogo wadogo na baadhi ya mawakala.

21. Kwa upande wa madawa ya Kilimo na Mifugo, upatikanaji haukuwa wa kuridhisha. Aidha ushuru unaotozwa kwenye madawa haya umechangia katika kupunguza uagizaji pamoja na matumizi kutokana na bei kuwa kubwa.

22. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuendeleza kilimo hiki. Kwa mfano miradi ya Mwamapuli yenye hekta 500 huko Tabora na Kitivo Tanga yenye hekta 640 imekamilika na zaidi ya wakulima 1,500 wanalima mpunga katika maeneo hayo. Aidha miradi ya Bahi - Dodoma na Chikuyu - Singida inayofadhiliwa na IFAD chini ya mpango wa kuendeleza kilimo cha majaruba ya mpunga imekamilika na wakulima wadogo wadogo wanalima kwenye eneo la jumla ya hekta 1000. Miradi ya Chomachankola - Tabora (600ha), Nsalala Shinyanga (150ha), Misungwi - Mwanza (70ha)

Chipanga - Dodoma (150ha), Lusilile- Singida (200ha) na Itumba - Tabora (150ha) iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

23. Mheshimiwa Spika, katika msimu huu kulitokea milipuko ya viwavijeshi, nzige na ndege waharibifu (Quelea quelea). Wizara yangu ikishirikiana na mashirika ya kimataifa ilijitahidi kudhibiti ndege na wadudu hawa wasilete uharibifu mkubwa. Aidha Wizara yangu iliendelea kudhibiti wadudu na wanyama waharibifu kwenye maghala na mashambani, kama dumuzi na kidung'ata.

24 Wizara pia imeiangalia upya sheria inayohusu karantini (Plant Protection 0rdinance) kwa lengo la kuimarisha udhibiti wa uingizaji na utoaji wa mazao, mimea na mifugo. Kijitabu cha mwongozo kinachohusu "Taratibu za Uingizaji wa Mbegu na Mimea Tanzania" kimechapishwa na usambazaji wa nakala 10,000 za awali unaendelea.

25. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utafiti vituo vyetu vilifanikiwa kuzalisha mbegu bora mpya za maharage aina ya Selian 94, Uwele - Okoa na Shida, na Ufuta - Ziada 94. Aidha vituo hivyo vilishiriki katika kutathmini ubora wa mbegu za mahindi zilizozalishwa na kampuni binafsi za mbegu. Vile vile utafiti wa mifugo uliendelea kutafuta mbinu za ufugaji bora wa mbuzi wa maziwa katika mikoa yenye matatizo ya ardhi ya Arusha na Kilimanjaro.

Kwa upande wa utafiti wa udongo ripoti za uchunguzi wa udongo wa vijiji vya Kabirizi na Nyankere wilaya ya Bukoba, mradi wa Kapunga mkoani Mbeya na mashamba ya mbegu za minazi huko Zanzibar umekamilika. Ripoti hizo zitatumika katika kutayarisha mapendekezo ya matumizi ya ardhi, mazao yanayofaa kulimwa pamoja na mahitaji ya mbolea katika maeneo hayo. Maeneo ya Kalulu na Manza Bay wilaya ya Muheza na maeneo ya Mwakinyumbi - Korogwe pia yanafanyiwa uchunguzi.

26. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho hicho wakulima 3500 walipata mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali za kilimo na ufugaji katika vyuo vyetu. Aidha wataalam 1071 walijiunga na mafunzo, kati ya hao 601 ni wa Astashahada na 470 wa Stashahada.

27. Tathmini ya shughuli za mafunzo, ukubwa wa vyuo, mwelekeo na mahitaji ya wataalam kwa sasa na baadaye imefanyika kwa msaada wa FAO na taarifa hiyo inapitiwa na wataalam wa Wizara yangu kwa maamuzi ya utekelezaji.

28. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo ya Ushirika uandikishaji wa vyama vya msingi 4,480 vyama vikuu 37, vyama 5 vya vilele (Apex organisation) viliandikishwa na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania liliundwa na kuandikishwa rasmi Desemba, 1994. Aidha ukaguzi wa vyama 2,083 ulifanyika.

29. Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililielezea Bunge lako kuwa kutokana na matatizo ya kisheria, utekelezaji wa ahadi ya serikali kuchukua madeni ya vyama vya ushirika yaliyotokana na maagizo yake ulichelewa. Napenda kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kuwa serikali imekamilisha suala hili, na imechukua madeni yote yaliyohusika.

30. Wizara yangu ikishirikiana na International Cooperative Alliance - (ICA), Chuo cha Ushirika na Rabo Bank ya Uholanzi imekamilisha maandalizi ya kuanzisha benki za ushirika. Benki ya Ushirika ya mkoa wa Kilimanjaro (Kilimanjaro Cooperative Bank Limited) imeandikishwa na inasubiri leseni toka Benki Kuu na vyama vikuu katika mikoa ya Kagera, Mwanza, Arusha na Tabora viliendelea na maandalizi ya kujiundia benki zao za Ushirika.

31. Mheshimiwa Spika, mwaka jana mwishoni serikali iliamua kukabidhi baadhi ya hisa za viwanda vya kukoboa kahawa vya mbozi na mbinga kwa wakulima wa kahawa. Hivi sasa taratibu za kukabidhi asilimia 65 ya hisa hizo kwa wakulima wa kahawa kwa kupitia chama cha kilele cha kahawa zinaendelea kukamilishwa na serikali.

32. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 1994/95 Wizara yangu ilianza kutekeleza sera mbalimbali zikiwemo za kuwashirikisha wafanyabishara na watu binafsi katika biashara ya mazao, pembejeo, madawa ya kilimo na mifugo na urekebishaji wa mashirika ya umma yaliyo chini ya wizara. Kwa kuwa mabadiliko hayo ni mapya miongoni mwa wakulima, wafugaji na wafanyabiashara kumekuwepo mafanikio na vile vile matatizo ya hapa

na pale.

33. Kwa upande wa ununuzi wa mazao ya biashara kumekuwepo na mafanikio katika ongezeko la bei kwa mkulima karibu kwa mazao yote na wakulima wamelipwa bila kucheleweshwa. Pamoja na kwamba utaratibu huu umeanza hivi karibuni tu lakini dalili zinaonyesha kuwa kutakuwepo ongezeko la uzalishaji na hii itajitokeza mapema kwa zao la pamba, tumbaku na korosho.

34. Pamoja na mafanikio kuwepo kuna matatizo yaliyojitokeza yakiwemo kukosekana takwimu sahihi za ununuzi wa mazao, ugumu wa utozaji ushuru wa mazao, na uchanganyaji wa mazao bila kuzingatia ubora hasa kwa wafanyabiashara wasio na uzoefu wa kutosha. Ili kukabili matatizo hayo Bodi husika zitaimarisha usimamizi pamoja na kurekebisha vipengele vya kanuni za ununuzi na uuzaji mazao nje ili kuwabana wahusika kisheria.

35. Kama nilivyoeleza kumekuwepo na mafanikio katika mwaka wa kwanza wa kuwaruhusu watu binafsi kuingiza mbolea nchini kiasi kwamba upatikanaji ulifikia asilimia 80%. Aidha waagizaji wa madawa ya mifugo nao wameonyesha nia ya kuagiza na kusambaza dawa kwa wafugaji. Tatizo ambalo linajitokeza katika eneo hili ni bei kubwa ya mbolea na dawa za mifugo kiasi kwamba uuzaji wake kwa wakulima na wafugaji unakwenda pole pole sana. Hali hii haitoi changamoto kwa waagizaji. Kwa hiyo Wizara yangu inachambua kuona ni njia zipi zitaweza kusaidia kushusha bei ya pembejeo hizi ikiwemo suala la ruzuku, kodi mbalimbali, utumiaji mfuko wa pembejeo nk.

36. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inayo mashirika mbalimbali yanayojishughulisha na uzalishaji yakiwemo ya chakula, chai, sukari, mkonge nk. Mashirika haya ni tofauti sana na mashirika ya viwanda kutokana na milki kubwa ya maeneo ya ardhi. Hivyo urekebishaji wa mashirika haya unaendelea chini ya Kamisheni ya Urekebishaji Mashirika ya Umma (PSRC) kwa kuzingatia tofauti hii. Suala la wakulima na wafanyakazi kupewa kipaumbele katika milki za mashirika yenye uhusiano wa moja kwa moja na mazao yao utazingatiwa katika ubinafsishaji na urekebishaji wa mashirika hayo.

37. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1994/95 Wizara na mashirika yake vilitengewa jumla ya shilingi 7,556.2 milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 11,297.9 milioni kwa ajili ya mpango wa maendeleo, fedha za hapa zikiwa shilingi 750 milioni na fedha za nje shilingi 10,547.9 milioni. Hadi kufikia Mei,1995 matumizi halisi ya fedha za mpango wa maendeleo yalikuwa shilingi 526.3 milioni ambazo ni asilimia 70 ya fedha za hapa na inatarajiwa kuwa fedha zote zitakuwa zimetumika ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha. Utekelezaji haukufikia malengo kutokana na mpango mzima kutoweza kupata fedha za maendeleo baada ya serikali kusimamisha utoaji wa fedha kwa kipindi cha Desemba 1994 hadi Aprili 1995.

## III. MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 1995/96

38. Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya Sera za Kijumla za uchumi na za Sekta, Wizara yangu imebakia na majukumu makubwa ya kutoa huduma muhimu za ushauri kwa wakulima, utafiti na mafunzo, pamoja na uandaaji na utekelezaji wa sera. Mpango wa Maendeleo wa mwaka 1995/96 unalenga katika kuimarisha na kuboresha majukumu muhimu ya Wizara ya Kilimo yafuatayo:

- Kuendeleza huduma ya elimu na ushauri kwa wakulima na wafugaji kwa kuzingatia mifumo ya kilimo na hali ya hewa kufuatana na maeneo.
- Kufanya utafiti wa mazao na mifugo na kusambaza matokeo ya utafiti huo haraka kwa wakulima.

- Kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea na mifugo, pamoja na kusimamia kikamilifu sheria zilizopo.

- Kutoa mafunzo ya kilimo bora kwa wataalamu wa kilimo, wakulima na wafugaji ili waongeze uzalishaji.

- Kuchambua, kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Kilimo na Mifugo.

! Kusimamia biashara huria hasa za mazao makuu.

! Kuimarisha Vyama vya Ushirika kwa kutoa ushauri.

! Kuendelea kuihamasisha sekta ya binafsi na kuishirikisha katika utoaji huduma za kilimo na mifugo.

! Kutoa ushauri wa uanzishaji wa Taasisi za Fedha vijijini (Rural Credit schemes).

39. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa 1995/96 utaendelea kutekelezwa katika mazingira magumu ya kiuchumi, hasa ikizingatiwa kuwa mpango wa mwaka 1994/95 haukuweza kutekelezwa kikamilifu kama ilivyotarajiwa kutokana na upungufu wa fedha. Hivyo katika mpango wa 1995/96, Wizara yangu itaweka mkazo katika kukamilisha shughuli zilizoanza mwaka uliopita.

Huduma za Ushauri kwa Wakulima na Wafugaji

40. Mheshimiwa spika, kwa kipindi cha miaka saba sasa Wizara yangu imekuwa ikiendesha mradi wa kuimarisha ushauri kwa wakulima na wafugaji (National Agriculture and Livestock Extension Rehabilitation Project - NALERP) na mradi huu sasa unafikia mwisho wa awamu yake ya kwanza Juni, 1996. Hivi sasa awamu ya pili ya mradi huu inaandaliwa ili kuendeleza shughuli za ushauri kwa wakulima na wafugaji. Awamu hiyo itajaribu kutatua matatizo ambayo hayakutatuliwa na awamu ya kwanza na pia kuendeleza yale ambayo hayakukamilika. Baadhi ya maeneo muhimu yatakayoshughulikiwa ni pamoja na kuwaimarisha wataalam kiujuzi, kuendelea kuwapatia nyumba na vitendea kazi, kuwapatia wakulima mafunzo na baadhi ya pembejeo muhimu na masuala ya hifadhi ardhi, mazingira na umwagiliaji yatapewa kipaumbele. Maeneo mengine yatakayohusika ni udhibiti wa magonjwa ya mifugo na mimea, malisho na afya ya mifugo, matumizi bora ya ardhi na uendelezaji wa matumizi ya zana bora za kilimo.

41. Miradi ya NALERP, IFAD-Southern Highlands Extension and Rural Financial Services, IFAD - Small holder Irrigation for Marginal Areas,

Sasakawa Global 2000, pamoja na miradi ya kuendeleza uzalishaji wa minazi, korosho kahawa na uendelezaji wa ng'ombe wa maziwa itaendelea kutoa huduma za ushauri na nyenzo zinazohitajika ili kuwafikia wakulima na wafugaji. Hivyo Wizara itaendelea kushirikiana kwa karibu na serikali na mashirika yanayosaidia miradi hii yakiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, EU, IFAD, WFP, Uholanzi na Uswiss.

42. Mheshimiwa Spika, Chama cha Kilimo (TASO) pamoja na wakulima wenyewe, kiko kwenye maandalizi ya sikukuu ya wakulima, yaani NANE NANE na maonyesho ya kilimo mwaka huu yatafanyika kitaifa huko Arusha. Hii itakuwa mara ya tatu mfululizo tangu maonyesho hayo yaanzishwe. Mwaka jana (1994/95) maonyesho na sherehe kama hizo zilifanyika kitaifa huko Morogoro. Sikukuu ya wakulima inaangalia mafanikio aliyoyapata mkulima na mfugaji kwa kipindi kilichopita na kujifunza mbinu mpya kutoka kwa wakulima wengine. Aidha wakulima hupata fursa ya kuona bidhaa na teknolojia mpya zilizoingia katika soko.

43. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa pembejeo umeanza rasmi Oktoba, 1994 baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha sheria Na 9 ya 1994 ya kuanzisha mfuko huo. Uongozi wa mfuko umeshakamilika baada ya Mtukufu Rais kumteua Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini na Waziri wa Kilimo kumteua Mkurugenzi Mtendaji pamoja na wajumbe wa Bodi. Bodi hiyo imekwishaanza kazi ya kutafuta fedha kwa ajili ya mfuko huo. Aidha kwa kutambua umuhimu wa mfuko wa pembejeo katika kuboresha hali ya kilimo nchini, serikali nayo imetenga shilingi 3.0 bilioni katika bajeti ya mwaka huu kama mchango wake. Kazi kubwa inayofanywa hivi sasa ni kuandaa taratibu za uendeshaji na usimamizi wa mfuko ikiwa ni pamoja na ukopeshaji na ukusanyaji wa madeni. Taratibu hizi zitakuwa zimekamilika na kuanza kutumika katika mwaka 1995/96.

44. Wizara yangu itaendelea kuhamasisha makampuni na taasisi mbali mbali katika sekta ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora, ili kuhakikisha upatikanaji wa mbegu zilizothibitishwa kwa wakulima. Inatarajiwa kuwa upatikanaji wa mbegu bora utafikia jumla ya Tani 6,027, za mbegu mbalimbali. Kampuni ya TANSEED inatarajia kuwa na jumla ya Tani 2,767 na kampuni ya CARGILL itazalisha jumla ya Tani 3,260 za mbegu. Matarajio haya ya upatikanaji kwa kampuni zote mbili yatakuwa

ni sawa na asilimia 45 ya makadirio ya mahitaji yote ya mbegu nchini ambayo ni karibu tani 12,800 kwa mwaka. Wizara yangu itaendelea kukamilisha na kutekeleza sera ya uzalishaji wa mbegu bora itakayohusisha wakulima wenyewe. Hii itasaidia ongezeko la upatikanaji mbegu, elimu na teknolojia ya mbegu kwa wakulima na uongezekaji wa mavuno kwa eneo.

45. Uwezo wa wananchi kununua zana bora za kilimo umepungua sana, hasa kutokana na pato dogo na kushuka kwa thamani ya fedha yetu. Hivi sasa inakadiriwa kuwa asilimia 10 tu ya wakulima wanalima kwa kutumia matrekta, asilimia 20 wanatumia wanyamakazi na wakulima wengi waliobaki wanatumia jembe la mkono. Hivyo Wizara yangu itaendelea kuweka mkazo katika matumizi ya zana zinazokokotwa na wanyama ili kuongeza tija katika kilimo kwa kutoa taaluma na ushauri kwenye vituo vya wanyamakazi.

## Umwagiliaji Mashamba

46. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha uandaaji wa mpango wa uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji hapa nchini "National Irrigation Development Plan". Mpango huu umechambua uwezo mkubwa uliopo nchini mwetu wa kuendeleza kilimo hiki kwa kutumia mabonde ya mito, vijito, maziwa na mabwawa na kuweka mikakati ya uendelezaji yenye uwiano mzuri na matumizi mazuri ya rasilimali tuliyonayo. Hivyo mpango wa maendeleo kwa mwaka 1995/96 utaweka umuhimu katika kutekeleza mikakati ifuatayo ili kuendeleza kilimo hiki:

- Kutoa ushauri katika uimarishaji na ukarabati wa miradi midogo midogo ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo wadogo.

- Kuendeleza kilimo cha mpunga kwa kutumia majaruba, hususan katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza.

- Kusaidia kuanzisha miradi midogo midogo ya umwagiliaji pamoja na kuwahamasisha wakulima kuunda vikundi na kupewa

mafunzo ya namna bora ya kutumia maji mashambani (Water Users Associations)

47. Katika jitihada ya kuoanisha matumizi bora ya maji katika mabonde ya mito Rufiji na Pangani, ambayo yote yana ushindani wa matumizi ya maji kati ya kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa nguvu za umeme, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Nishati na Madini, kwa msaada wa fedha kutoka Benki ya

Dunia inatayarisha mpango wa matumizi bora ya maji katika mabonde haya. Matayarisho ya mradi yameanza na yanategemewa kukamilika mwaka wa fedha wa 1995/96.

48. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kutoa huduma na ushauri katika kuendeleza mifereji ya jadi katika mikoa ya Kilimanjaro, Tanga na Arusha pamoja na ile ya Usangu, Madibira na Pawaga. Sambamba na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji, Wizara itaendelea kuhamasisha na kutoa mafunzo ya namna bora ya kutumia maji ya umwagiliaji pamoja na kuimarisha umoja wa watumiaji ili kuwawezesha kujitegemea katika uzalishaji, uendelezaji na utunzaji wa miradi yao ya umwagiliaji. Hii itasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao kwa kuzingatia njia bora za kilimo, hifadhi ya mazingira pamoja na kulinda afya za wakulima wenyewe.

Utafiti wa Mazao ya Kilimo na Mifugo

49. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mradi wa kitaifa wa utafiti wa kilimo na mifugo (National Agriculture and Livestock Research Project) katika kusaidia kutatua matatizo yanayowakabili wakulima na wafugaji. Umuhimu utawekwa katika kukarabati vituo vya utafiti pamoja na kuvipatia vitendea kazi, ili utafiti wa mazao makuu ya chakula na biashara uweze kuendelea vizuri. Aidha katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo Wizara itaendelea na utafiti wa uzalishaji wa aina bora ya mifugo yenye kutoa nyama na maziwa kwa wingi pamoja na utafiti wa namna ya kuongeza malisho na lishe kwa mifugo.

50. Katika kuongeza ufanisi wa utafiti wa udongo, Wizara yangu imekamilisha utayarishaji wa rasimu ya kwanza ya kijitabu cha mwongozo

wa kuchunguza udongo na kutathimini matumizi ya udongo. Mkazo utawekwa katika kutafiti utumiaji bora wa mbolea za asili, kuendelea kufanya uchunguzi wa udongo (Soil Survey) na kuangalia mpangilio mzuri wa matumizi ya mfumo wa ardhi na tathmini yake.

51. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha uwiano kati ya utafiti wa kilimo na mifugo na ushauri kwa wakulima na wafugaji, sehemu ya utafiti wa mifumo ya kilimo na ufugaji (Farming System Research) itawahusisha wakulima na mabwana shamba kikamilifu katika kubuni na kusambaza teknolojia zinazozingatia matatizo na mazingira ya wakulima wenyewe. Azma hii itatimizwa kwa kuendelea kufanya majaribio yanayowahusu wakulima moja kwa moja katika kanda zote za utafiti. Wizara vile vile itazingatia utatifi wa mifumo ya kilimo na ufugaji kwa kuzingatia masuala ya kijamii hasa yale ya kijinsia na masuala yanayohusu utumiaji mzuri wa maliasili.

52. Utafiti wa magonjwa ya mifugo kwa lengo la kupata mbinu bora za kudhibiti maradhi ya mifugo ambayo yametokea kuzuka mara kwa mara utaendelezwa katika maeneo yafuatayo:

! Kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu katika ng’ombe (CBPP). Maabara zetu zinaendelea kufanya uchunguzi wa ubora wa chanjo na namna ya kuzuia ugonjwa huu.

! Kutathmini chanjo ya Ndigana Kali (ECF) ambayo matumizi yake yanazidi kupanuka nchini. Lengo ni kukinga mifugo yote dhidi ya Ndigana Kali, tukianzia na ng’ombe wa maziwa.

! Kufanya uchunguzi wa mimea yenye sumu inayoathiri mifugo, hasa katika mikoa ya kusini. Lengo ni kupunguza vifo vya ng’ombe kutokana na kula mimea yenye sumu kali.

Mafunzo na Ajira ya Wataalam

53. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafanya zoezi la kutathmini shughuli zote za mafunzo, ukubwa wa vyuo ili kuwa na mwelekeo na

mahitaji halisi ya wataalamu wa kilimo, mifugo na ushirika, kwa sasa na baadaye. Uchambuzi huu wa mafunzo una lengo la kutoa mafunzo yatakayolingana na mabadiliko ya Sera ya Uchumi nchini. Wizara itaweka mkazo katika kutoa mafunzo kwa wahitimu yanayolenga katika kujitegemea na kujiajiri wenyewe katika sekta ya kilimo na ufugaji, badala ya mafunzo yanayotegemea ajira ya serikali.

54. Mbali na kwamba liko tatizo la fedha na ajira, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake na wanafunzi watarajali (Pre-service) walau kwa kiwango kidogo ili kukidhi mahitaji ya kujaza nafasi chache zitakazokuwa wazi serikalini na kwenye taasisi za watu binafsi.

55. Katika juhudi za kutoa mafunzo kwa wataalam, hivi sasa kuna wanawake wachache wanaojiunga na mafunzo ya kilimo na mifugo baada ya elimu ya Sekondari. Kwa kuwa idadi kubwa ya wakulima vijijini ni wanawake, Wizara yangu kwa kutumia vyuo vyake itaendelea kuwahamasisha wanafunzi wa kike wajiunge na mafunzo na baadaye waweze wao wenyewe kuwa wakulima/wafugaji bora na pia waweze kutoa ushauri kwa wenzao.

Udhibiti wa Magonjwa, Wadudu na Ndege Waharibifu wa Mimea na Mifugo

56. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kutoa huduma ya kudhibiti magonjwa na viumbe waharibifu wa mazao na mifugo. Huduma hii italenga katika kudhibiti magonjwa, wadudu na ndege waharibifu wanaosababisha uharibifu mkubwa wa mazao na mifugo. Milipuko ya namna hii haiwezi kudhibitiwa na mkulima mmoja mmoja, wala uwezo wetu wenyewe hauwezi kukidhi jambo hili. Hivyo Wizara yangu pamoja na uwezo wake mdogo uliopo itaendelea kushirikiana na mashirika ya kimataifa ili kupambana na milipuko hii.

57. Ili kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea na mifugo kwa udhibiti kibailojia na udhibiti husishi (Biological Control & Integrated Pest Management), pamoja na uharibifu wa mazao ghalani ambao unakisiwa kusababisha upotevu kwa asilimia 30 - 40, Wizara itaendeleza shughuli muhimu zifuatazo:

- Kuendeleza kampeni ya kuangamiza dumuzi katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

- Kusambaza madawa ya hifadhi ya mazao kwa wakulima mikoani.

- Kuendeleza utoaji wa mafunzo ya hifadhi ya mazao kwa mabwana shamba na wakulima.

- Kuendelea na utunzaji wa shamba la mbegu ya mihogo linalotumika kuzalisha wadudu maadui wa Kidung'ata wa Muhogo.

- Kusimamia kikamilifu sheria ya uingizaji na utoaji nje mimea, mifugo na bidhaa zinazohusika.

Kilimo na Hifadhi ya Mazingira

58. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inahimiza kilimo kinachozingatia hifadhi ya mazingira kwa kutoa elimu na ushauri kwa wakulima na wafugaji juu ya hifadhi ya udongo na maji na kusisitiza kilimo cha mseto (agroforestry). Aidha utekelezaji wa programu ya taifa ya hifadhi ya udongo na maji umeanza katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Morogoro na Iringa. Ili kupata mwelekeo mzuri wa utekelezaji wa Programu hii, Wizara imeanza zoezi la kuratibu miradi yote ya hifadhi ya mazingira hapa nchini ili kujua idadi yake, maeneo ilipo, utendaji wake wa kazi, watekelezaji na tekinolojia inayotumika. Kazi ya usimamizi na utekelezaji ni jukumu la mikoa na serikali za mitaa zinazohusika.

Maendeleo ya Ushirika

59. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo ya Ushirika, baada ya kuandikishwa upya Vyama vya Ushirika, msukumo mkubwa unaendelea kuelekezwa kwenye mafunzo kazini kwa watumishi pamoja na Halmashauri za Vyama vya Ushirika. Mbinu za kuongeza mitaji, kuanzisha na kuendeleza mifuko ya ununuzi wa mazao na pembejeo mbalimbali, na uanzishaji wa benki za ushirika zitaendelea kutolewa.

60. Kama nilivyodokeza awali Wizara yangu ikishirikiana na ICA - Moshi, Chuo cha Ushirika Moshi na Rabo Bank ya Uholanzi imekamilisha utafiti wa uanzishaji wa benki ya ushirika na mapendekezo yake yatatumika kuwashawishi wanaushirika jinsi chombo hiki cha fedha kitakavyowakwamua kutokana na madeni makubwa ya mabenki. Katika kutekeleza taratibu za kuanzisha Benki za Ushirika, mkoa wa Kilimanjaro, wenye vyama hai vya Akiba na Mikopo umechukua nafasi ya kwanza na tayari una Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro. Maeneo mengine ambayo yameanza kutekeleza taratibu za kuanzisha Benki za Ushirika lakini bado kuzisajili ni Arusha, Mwanza, Kagera na Tabora. Sekta ya Benki ni nyeti na hatutegemei kuwa na mlipuko wa Benki za Ushirika nchini zenye misingi hafifu ya kiuchumi. Hivyo Wizara yangu itakuwa makini sana kutoa ushauri wa kitalaam kwa Vyama vya Ushirika pale unapohitajika ili kuhakikisha kuwa vyama hivi vinakuwa ni vitovu halisi vya uchumi vyenye lengo la kumwendeleza mkulima/mfanyakazi/mwanachama.

61. Pamoja na kuwepo sera za kushirikisha makampuni na watu binafsi katika shughuli za biashara ya mazao na pembejeo, bado Ushirika unamiliki karibu asilimia 96 ya soko hili. Kutokana na ukweli huu, napenda kulitumia Bunge lako Tukufu kuwashauri wanaushirika nchini kuongeza nguvu na mbinu zao hasa katika sekta ya biashara wakishirikiana na viongozi na menejimenti ya vyama vyao. Mafanikio mazuri yanaweza kupatikana endapo wanaushirika watatumia kwa ukamilifu na kwa ufanisi zaidi nyenzo walizonazo wenyewe. Kwa mfano uanzishaji na usimamizi mzuri wa mifuko ya ununuzi wa mazao na pembejeo iliyoandikishwa kisheria ili kulinda fedha za wanachama, uanzishaji na uimarishaji wa vyama vya akiba na mikopo, mabenki ya ushirika na kadhalika. Hata hivyo ni muhimu sana kwa watendaji na Halmashauri za Vyama vya Ushirika kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kupunguza gharama za uendeshaji ili wanachama waone umuhimu wa kutumia ushirika wao.

## Sera na Mipango ya Kilimo

62. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendeleza mipango na programu za sekta zinazozingatia sera za ujumla na za sekta. Kwa mwaka 1995/96 majukumu muhimu katika sekta ya kilimo yatakuwa kama ifuatavyo:

- Kuwasilisha serikalini Sera ya Kilimo na Mifugo ambayo uhuishaji wake umekamilika.

- Kukamilisha sensa ya kilimo na mifugo kwa kushirikiana na idara kuu ya Takwimu.
- Kukamilisha uchambuaji wa majukumu ya Wizara na kurekebisha muundo ili kuwianisha na majukumu makuu ya serikali.

- Kuratibu na kutathmini shughuli za sekta binafsi katika ununuzi wa mazao na pembejeo.

- Kutayarisha mikakati ya muda wa kati ya kuendeleza kilimo nchini (Medium Term Development Strategy).

- Kutayarisha programu ya muda wa kati ya uwekezaji katika Sekta ya Kilimo (Medium Term Sectoral Investment Programme).

- Kuendelea kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma katika zoezi linaloendelea la kuangalia upya miundo ya Mashirika na ubinafsishaji.

- Kuanzisha mfuko wa kinga (stabilization fund).

Maendeleo ya Watumishi

63. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea na zoezi la kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu sahihi za watumishi ili zitumike katika kushughulikia maslahi mbalimbali ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuwapandisha vyeo na kuthibitishwa kazini katika muda unaotakiwa. Katika kipindi cha mwaka 1994/95 watumishi 2,500 wamethibitishwa kazini na watumishi 14,020 wamepandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali.

64. Katika Mpango wa 1995/96 Wizara itaendelea kuangalia maslahi ya watumishi na inatarajia kuwathibitisha na kuwapandisha vyeo watumishi zaidi ya 400 katika ngazi ya KAMUS; watumishi 5,704 katika ngazi ya TUMEAJIRI, na watumishi 22 katika ngazi ya Mamlaka ya RAIS. Wizara

itaongeza juhudi zaidi kuwaondolea usumbufu wataalam wetu ili wawe wanathibitishwa na kupandishwa vyeo katika muda unaotakiwa. Kwa niaba ya Wizara yangu napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Idara Kuu ya Utumishi, pamoja na Tume ya Utumishi Serikalini (TUMEAJIRI) kwa ushirikiano wao katika kufanikisha zoezi hili.

## IV. MAJUMUISHO

65. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi kubwa yenye watu, rasilimali nyingi, hali ya hewa nzuri na imejaliwa kuwa na mazingira ya amani na utulivu lakini ni nchi masikini sana. Katika mazingira haya umasikini wa Tanzania hauna msingi. Aidha tumeimba umasikini wa Tanzania na kuusisitiza mara nyingi kiasi kwamba kila mwananchi anadhani umasikini huu ni sehemu ya kudumu ya utamaduni wetu. Tukitaka kujikwamua kutoka umasikini huu, ni lazima kwanza tujikomboe, kutoka katika fikra potofu ya kudhani umasikini ni sehemu ya maisha yetu. Ili tufanikiwe katika lengo hili ni lazima tujenge mazingira sasa ya kila Mtanzania kufikiri, kuzungumza na kutenda namna ya kuongeza utajiri wa Mtanzania na siyo namna ya kukabiliana na umasikini wa Mtanzania kila siku.

66. Suala kubwa iwe ni tufanye nini ili nchi yetu iwe tajiri. Ili kujibu swali hili kwanza lazima tujue kwanini imekuwa masikini. Napenda niwakumbushe wimbo wetu mwigine ambao kila mwananchi anauimba nao ni kuwa “Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu”. Usemi huu ni wa kweli na hauna mjadala kwa sababu idadi kubwa ya Watanzania zaidi ya asilimia 80 hutegemea kilimo, kilimo ndicho kinaajiri watu wengi na sehemu kubwa ya mapato ya fedha za kigeni zaidi ya asilimia 70 zinatokana na mauzo ya bidhaa za kilimo. Kama kilimo ndicho kimekuwa kikitegemewa na kuchangia katika uchumi kwa viwango nilivyovitaja, basi bila shaka ni kweli kuwa kilimo ndicho kilichotufanya tukawa masikini. Kama hii ni kweli, basi bila shaka pia ni kweli kuwa kilimo ndicho kitakachotutoa katika umasikini na kutuingiza katika utajiri. Mimi ninaamini hakuna njia ya mkato ya kuukwamua uchumi wa nchi hii isipokuwa kwa njia ya kuongeza na kuimarisha uzalishaji katika kilimo. Kilimo kwa miaka mingi inayokuja kitaendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi na “engine” ya maendeleo ya nchi nii. Sekta zingine zote zinafanya kazi ya kukisaidia tu kilimo ili mafanikio yapatikane kwa haraka zaidi.

67. Mheshimiwa spika, labda tuangalie ilikuwa nini hasa mpaka tukafikia hali hii. Katika miaka ya mwanzoni mawa 1970 Tanzania ilikuwa na watu kama milioni 14.5 (1993). Leo Tanzania ina watu milioni 27, karibu mara mbili ya idadi ya watu ya mwaka 1973. Wakati idadi ya watu inaongezeka kwa kasi hivyo uzalishaji wa mazao yetu makuu umekuwa unashuka kwa kasi sana au haukuongezeka. Kwa mfano, uzalishaji wa katani ulipungua kutoka zaidi ya tani 220,000 mwaka 1964 hadi tani 33,000 leo. Uzalishaji wa korosho ulipungua kutoka tani 114,000 mwaka 1973/74 hadi tani 17,000 mwaka 1987/88, na hivi leo uko tani 60,000. Ninapenda niwapongeze wakulima wa korosho japo hawajafikia kiwango cha zamani wakati idadi yao ilipokuwa nusu. Uzalishaji wa mazao mengine makubwa ya kahawa, pamba, tumbaku n.k. umekuwa unapanda na kushuka lakini wastani wake ni wa viwango vya miaka ya 1965 - 1975.

68. Mheshimiwa Spika, katika mazingira haya utakwepa vipi kuwa masikini? Leo kipato cha Mtanzania ni US$ 130. Taarifa zingine za Benki ya Dunia zinaonyesha pato la Mtanzania lilishawahi kufikia US$320. Katika dunia hii sehemu masikini sana na yenye matatizo ya kutisha ni Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Pato la wastani katika eneo hilo ni US$340. Pato la Mtanzania ni karibu theluthi moja tu ya pato la masikini hawa, na liko chini kabisa ya pato linalohitajika kumfanya binadamu aishi kwa viwango vya umoja wa mataifa. Katika hali hiyo tujiulize: Hivi Tanzania itakuwa kinara wa umasikini mpaka lini? Natambua kuwa haya siyo mambo mazuri kuyasikia lakini ni vema tukayafahamu.

69. Kama tunataka kuondokana na hali tuliyoko sasa, ni lazima tuelekeze fikra zetu, macho yetu, nguvu zetu na rasilimali zetu katika kilimo. Wizara yangu itaivalia njuga kazi hii hadi mafanikio yatakapopatikana. Napenda nieleze wazi kuwa kubadili jambo lililoota mizizi kama utamaduni siyo kazi rahisi. Kama nilivyosema awali itahitaji mageuzi ya fikra, kujitolea sana, kujitosa kwingi, uwekezaji rasilimali kwa wingi na zaidi ya yote uelewa na ushirikiano wa kila mmoja wetu. Nguvu kubwa lazima ielekezwe katika uzalishaji na hasa kwa wakulima wadogo. Kazi hii iwe ni agenda ya kila mmoja kama tunataka mafanikio ya haraka. Uwezo wa kujikwamua uko mikononi mwetu, kwa wananchi wetu na wala tusitazame pembeni.

70. Wizara yangu inatambua uwezo mdogo wa serikali kugharimia peke yake shughuli hizi muhimu za kuibua na kuinua viwango vyetu vya uzalishaji wa mazao ambavyo viko chini. Kwa sababu hiyo, Wizara inaona kama tunataka kupata mafanikio ya haraka ni lazima wahusika wengine katika shughuli hizi nao wachangie nguvu za serikali. Maeneo muhimu yatakayohitaji michango hiyo ni utafiti, ushauri, pembejeo muhimu na inapobidi kuanzisha mifuko ya kinga (stabilization funds). Ili kufanikisha azma hii, Wizara itaanzisha mifuko hii maalum kwa mwaka huu kwa mazao makuu matatu ya kahawa, pamba, na korosho. Zao la kahawa linategemewa kukusanya shilingi 1.0 bilioni pamba shilingi 1.0 bilioni na korosho shilingi 0.5 bilioni. Fedha hizi zinazokusanywa zitatumika kwa maendeleo ya zao linalohusika na zitakusanywa na Bodi ya zao katika soko la mwisho. Aidha mazao mengine yataingizwa katika utaratibu huu katika misimu inayofuata. Ni tegemeo langu kuwa wakulima, vyama vya ushirika na wanunuzi wa mazao yetu wataona umuhimu wa hatua hii na kushiriki kikamilifu. Taratibu za namna ya kuendesha mifuko hii zinakamilishwa.

## V. SHUKRANI

71. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa yanayoendelea kutusaidia katika juhudi zetu za kuendeleza kilimo, mifugo na ushirika. Ningependa kuzishukuru nchi zifuatazo kwa misaada yao: Australia, Canada, China, Denmark, Finland, India, Iran, Italia, Japan, Jamhuri ya Watu wa Korea, Marekani, Norway, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Uswiss, Uholanzi na Ufaransa. Aidha ningependa kuyashukuru mashirika na Taasisi za kimataifa kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, CILCA, EADB, EU, FAO, HPI, IDRC, IFAD, Sasakawa Global 2000, UNDP, WFP na UNICEF.

72. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wakulina na wafugaji wote wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Bila juhudi zao Watanzania wasingekula na uchumi wa nchi hii ungekuwa katika hali mbaya zaidi ya ulivyo sasa. Ukombozi wa uchumi wa nchi hii uko mikononi mwa wakulima hawa na hasa wale wadogo wadogo. Napenda niwashukuru kwa niaba ya Watanzania wote. Pili napenda nimshukuru Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Njelu M.Kasaka, Mb. na ninamtakia mafanikio mema

katika uchaguzi wa mwaka huu. Tatu napenda nimshukuru sana Ndugu Raphael Mhagama, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo pamoja na watumishi wote wa wizara na mashirika yote yaliyo chini ya wizara kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuandaa makisio haya na kutayarisha maelezo yote kuhusu bajeti hii, na mwisho napenda nimshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii.

## VI. MAOMBI YA FEDHA

73. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 11,598.96 milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 5,598.536 milioni kwa ajili ya shughuli za maendeleo, shilingi 945.9 milioni zikiwa ni fedha za hapa na shilingi 4,652.636 milioni zikiwa ni fedha za kigeni.

74. Mheshimiwa Spika, hiki ni kikao cha mwisho cha Bunge hili. Baada ya kikao hiki Bunge litavunjwa na wengi wetu tutakuwa katika harakati za kutafuta namna ya kurudi tena Bungeni na wachache wetu katika harakati za kuwania nafasi ya Urais. Napenda niwapongeze sana Waheshimiwa Cleopa David Msuya, Benjamin William Mkapa na Jakaya Mrisho Kikwete kwa kufanikiwa kuvuka kiunzi cha kwanza salama na kuteuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM kwenda katika Mkutano Mkuu kuwania nafasi ya ugombea Urais kwa kiti cha CCM. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawatakia Waheshimiwa Wabunge wote kila la kheri katika harakati hizo mbili.
Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

75. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.